# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 017

JUNI- SEPTEMBA, 2021




## Historia yaandikwa Shirati, ni mageuzi sekta ya maji

BAADA ya dhiki ni faraja. Ndivyo tunavyoweza kuielezea furaha ya maelfu ya wakazi wa mji mdogo wa Shirati wilayani Rorya, baada ya kurejeshewa huduma ya majisafi ya bomba kutoka Ziwa Victoria, ambayo wameikosa kwa kipindi cha wastani wa miaka sita.

Januari 6, mwaka huu 2021, Waziri Aweso alizuru Shirati, ambapo katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu Majaliwa, aliiagiza MUWASA kukarabati miundombinu ya mradi huo wa maji, ili kurejesha huduma kwa wakazi na wananchi kama ilivyokuwa awali.



## RUWASA lazima tuwe wa kisasa zaidi-Aweso

## Katibu Mkuu Maji Mhandisi Sanga akagua utendaji wa sekta ya maji Mtwara



# Historia yaandikwa Shirati, ni mageuzi sekta ya maji



BAADA ya dhiki ni faraja. Ndivyo tunavyoweza kuielezea furaha ya maelfu ya wakazi wa mji mdogo wa Shirati wilayani Rorya, baada ya kurejeshewa huduma ya majisafi ya bomba kutoka Ziwa Victoria, ambayo wameikosa kwa kipindi cha wastani wa miaka sita.

Wananchi hao licha ya kuwa jirani na watunzaji wa rasilimali maji ya ziwa hilo, walikosa huduma hiyo tangu mwaka 2015, kutokana na ubovu wa miundombinu ya mradi wa maji wa Shirati.

Hata hivyo, wataalamu wa Serikali kupitia Wizara ya Maji na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA), imefanikiwa kuhuisha mradi huo baada ya kukamilisha ukarabati wa miundombinu yake kwa asilimia 100.

"Tunaishukuru sana Serikali yetu kwa kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya mradi wa maji ya bomba, iliyokuwa imeharibika na kutukosesha maji kwa miaka sita. Sasa hivi wana-Shirati tunapata majisafi kama zamani, ni faraja kubwa sana," Mkazi wa Shirati, Stela Otieno anasema.

Mkazi mwingine wa mji huo, Monica Tisa anasema "Kero yetu kubwa ilikuwa maji, sasa tunapata huduma ya maji safi ya bomba, tunamshukuu sana Rais wetu Samia Suluhu Hassan na wote waliohusika katika kuturejeshea huduma hii muhimu, Mungu awabariki."

Mussa Okello ni mkazi wa Shirati pia. Anasema "Ufufuaji wa mradi huu wa maji umepunguza kwa asilimia kubwa ugomvi na migogoro ya ndoa miongoni mwa wananchi wa Shirati, kwa sababu wanawake walikuwa wanaondoka alfajiri kwenda kutafuta maji na kuchelewa kurudi nyumbani."

Chimbuko la urejeshaji huduma ya maji ya bomba katika mji wa Shirati umetokana na kazi za viongozi ambao ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (Mb) na Waziri wa Maji Jumaa Aweso (Mb), waliofanya ziara kwa nyakati tofauti katika mji huo wenye takribani zaidi ya wakazi 30,804, kwa mujibu wa sesa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

Januari 6, mwaka huu 2021, Waziri Aweso alizuru Shirati, ambapo katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu Majaliwa, aliiagiza MUWASA kukarabati miundombinu ya mradi huo wa maji, ili kurejesha huduma kwa wakazi na wananchi kama ilivyokuwa awali.

Siku hiyo hiyo, bila kupoteza wakati, Waziri Aweso aliahidi kuipatia MUWASA Sh milioni 247 kwa ajili ya kuanza ukarabati wa miundombinu hiyo, ahadi ambayo ilitekelezwa Januari 27, mwaka huu 2021.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa MUWASA kwa kipindi hicho, CPA Joyce Msiru, ukarabati wa miundombinu ya mradi huo ulianza baada ya ofisi yake kupokea fedha kutoka serikalini.
CPA Msiru anasema MUWASA imekamilisha utekelezaji wa mradi huo kwa asilimia 100, kwa gharama ya Sh milioni 493 zilizotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Maji.

Anasema ukarabati wa miundombinu ya mradi huo ulihusisha kazi mbalimbali, ikiwemo marekebisho ya mashine ya kusukuma maji (Pump) katika kituo cha Michire (yenye uwezo wa kusukuma maji kwa mita za ujazo 21 kwa saa) na nyingine yenye uwezo wa kusukuma maji kwa mita za ujazo 90 kwa saa.

Pia, marekebisho makubwa ya mabomba katika njia kuu ya kusafirisha maji kutoka kituo cha kusukuma maji cha Michire mpaka kwenye tenki la kuhifadhi maji lililopo katika kilele cha mlima Obhoke kwa urefu wa kilomita tano.

"Katika urefu huo, mabomba mapya yenye kipenyo cha milimita 200 yalilazwa kwa urefu wa mita 1,330. Ukarabati mwingine ni wa tenki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 1,500,000 lililopo eneo la mlima Obhoke na mfumo wa usambazaji maji kwa kuweka bomba mpya kwa urefu wa kilomita saba," CPA Msiru anaongeza.

Anasema hadi sasa wateja 602, wakiwemo 567 wa majumbani, sawa na wastani wa wakazi zaidi ya 5,000 wa mji wa Shirati, wanapata huduma ya maji ya bomba, kupitia tenki lenye ukubwa wa mita za ujazo 1,500.

CPA Msiru anasema MUWASA inaendelea kupokea maombi kutoka kwa wakazi wa vijiji vya Obwere, Michire, Obhoke, Ngasaro na Kabwana wanaohitaji kuunganishiwa huduma ya maji ya bomba katika makazi yao.

Anabainisha kuwa gharama za kuunganisha huduma ya maji ya mradi huo katika mji wa Shirati ni kati ya Sh 11,500 na 250,000 (kutegemea na umbali wa eneo la mteja kutoka bomba la kusambaza majisafi).

Mradi wa maji wa Shirati umeendelea kutembelewa na viongozi mbalimbali kuanzia wakati wa ukarabati hadi kukamilika kwake, wakiwemo Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (Mb).

Mwezi Agosti 2021, Waziri Aweso alikwenda kuzindua ukarabati wa miundombinu ya mradi wa maji unaotekelezwa na MUWASA katika mji wa Shirati.

Katika hotuba yake kwa wananchi waliofurika katika uwanja wa Obwere, mjini Shirati, Waziri huyo aliipongeza MUWASA, chini ya uongozi wa CPA Msiru kwa kazi nzuri ya kuhuisha mradi huo na kurejesha huduma ya maji kwa wananchi.

"Furaha yangu ni kuona wananchi wanapata majisafi na dhamira ya Rais wetu Samia Suluhu Hassan ni kumtua mama ndoo kichwani," alisema Waziri Aweso.

Waziri Aweso alitumia wasaa huo pia kumteua CPA Msiru kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usambazaji Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Wizara ya Maji , na kesho yake alimteua Meneja Ufundi wa MUWASA, Nicas Mugisha kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo.

"Dada yangu na Mkurugenzi [wa MUWASA] umeweza kuniheshimisha, kulikuwa na miradi kichefuchefu ambayo utekelezaji wake ulikuwa ni mgumu, mradi wa kwanza ni Mugumu [mradi wa maji wa Manchira wilayani Serengeti], kila mtu ambaye anautekeleza unamshinda, nimeweka vidume kweli kweli vimeshindwa.

"Lakini huyu mama nilivyomwambia nenda kautekeleze ule mradi, kwake ulikuwa siyo mgumu, lakini tumempa miradi mingi, leo tumekuja kumpa huu mradi wa Shirati, tulimpa siku 30, yeye amefanya kwa siku 21, nani kama Joyce ndugu zangu… huyu mama tumempa kazi ngumu, kila kazi tuliyompa ameweza kuikwamua.
"Kwa mamlaka niliyopewa na kuaminiwa na Rais wangu Samia Suluhu Hassan, ndugu yangu Joyce Msiru ninamteua kuwa Mkurugenzi wa mamlaka za maji zote nchini, kwa sababu hii kazi anaiweza," Waziri Aweso alisema na kushangiliwa na umati mkubwa mkutanoni hapo.

Akizungumzia uhuishaji wa mradi wa maji wa Shirati, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Wizara ya Maji, Florence Temba alisema "Mradi huu ni mafanikio ya kihistoria kwa wananchi wa Shirati, ikiwa ni utatuzi wa changamoto kubwa ya maji iliyowakili kwa muda mrefu."

Miongoni mwa viongozi waliofuatana na Waziri Aweso katika ziara hiyo ya Shirati, ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mara, Shaibu Ngatiche.

Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikoka na Mbunge wa Rorya, Jafari Chege, viongozi hao kwa nyakati tofauti katika hafla hiyo waliishukuru Serikali na kuhimiza wananchi na wakazi wote kulinda na kutunza miundombinu ya mradi wa maji katika mji wa Shirati ili uwe endelevu na kuwahudumia kwa kizazi cha sasa vizazi vijavyo kwa sababu huduma ya majisafi haina mmbadala na idadi ya watu na matumizi inaongezeka.

# RUWASA lazima tuwe wa kisasa zaidi-Aweso

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameuelekeza uongozi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuwa na mkakati wa kutumia vifaa vya kisasa katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Waziri Aweso amesema hayo wakati akipokea taarifa ya RUWASA kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji ya vijijini tangu ilipoanza kazi Julai 2019.

Agizo hilo amelitoa leo Septemba 09, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa Wizara ya Maji Jijini Dodoma.

Waziri Aweso alisema ni muhimu RUWASA ikawa na vifaa vyake vya kisasa ili kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maji, iweze kumaliza kwa wakati sambamba na kupunguza gharama kwa kuwatumia wakandarasi.

"Tunachohitaji ni kuona miradi inakamilika kwa wakati, Serikali ipo tayari kutoa fedha za kuhakikisha RUWASA inakuwa na vifaa vya kisasa kabisa," Waziri Aweso amesema.

Aidha, amesisitiza wataalamu kwenye Sekta ya Maji kuhakikisha wanatumia vyema taaluma zao ili falsafa ya kumtua Mama ndoo kichwani sambamba na kaulimbiu ya RUWASA ya "Maji bombani" itimie kikamilifu.

Wakati wa tukio hilo la upokeaji wa taarifa, Waziri Aweso alimuelekeza Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mhandisi Clement Kivegalo kufanya tathmini ya Wahandisi wa maji wa RUWASA ili kujiridhisha na weledi na utayari wao wa kuwafikishia wananchi huduma ya majisafi.

"Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amedhamiria kwa dhati kumtua mwanamama wa Tanzania ndoo kichwani, sasa ni muhimu tukazingatia hili na Mhandisi asiyekuwa na uwezo wa kazi aondolewe tuwaache wenye uwezo," Waziri Aweso alisisitiza.

Tukio hilo limehudhuriwa na Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb), Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga na wataalamu kutoka Wizara ya Maji.

RUWASA inafanya kazi katika mikoa 25 ya Tanzania.





*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea na uongozi wa RUWASA, pamoja na wataalamu wa Wizara ya Maji wakati akipokea ripoti ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.*

# Katibu Mkuu Maji Mhandisi Sanga akagua utendaji wa sekta ya maji Mtwara

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga mwishoni mwezi Septemba 2021 amefanya ziara ya kikazi na kukagua utendaji wa Sekta ya Maji mkoani Mtwara.

Mhandisi Sanga katika ziara hiyo amewataka watendaji na wataalamu wa sekta ya maji kutumia ubunifu katika kutoa huduma, na kuepuka gharama ambazo hazina ulazima.

Amesisitiza wataalamu kutumia usanifu wa miradi utakaowezesha majisafi kuwafikia wananchi kwa njia ya mserereko, hivyo huduma hiyo kumfikia mlaji kwa gharama ndogo.



*Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga akiongea na wanakijiji katika moja ya eneo la umma la kupata huduma ya maji wilayani Newala, Mtwara.*



*Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga akikagua ubora wa mmashine za kusukuma maji (pump), katika mradi wa maji wa Makonde, mkoani Mtwara*



*Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga akikagua chanzo cha maji cha Mbwinji kinachotumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi Nachingwea (MANAWASA) kusambaza huduma ya maji, (kulia) ni Mkurugenzi Mtendaji wa MANAWASA Mhandisi Nuntufye Mwamsojo*

# Miradi sita muarobaini wa changamoto ya Maji Mbeya

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2012, Jiji la Mbeya na Vitongoji vyake pamoja na Mji Mdogo wa Mbalizi lilikuwa na wa-kazi wapatao 600,000. Kwa sasa idadi hiyo inakisiwa kuwa imeongezeka hadi kufikia 809,000.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya CPA Gilbert Kayange anasema mamalaka anayoiongoza malengo yake ni kuhakikisha wanafikiwa na huduma ya majisafi na salama, na kwamba wamejipanga kuhakikisha malengo yanafikiwa kwa wakati.

"Mikakati iliyopo ni mizuri. Ni matumaini yetu kuwa changamoto ya upatika-naji wa majisafi katika maeneo yasiyo na huduma hiyo kwa sasa itasahauli-ka baada ya muda mfupi." Anasema Kayange wakati akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa miradi ya Maji kwa Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) wakati wa ziara aliyoifanya mkoani hapo mapema Julai 2021.

Kayange anasema kutokana na idadi hiyo, mahitaji ya maji ni wastani wa lita milioni 80 kwa siku. Mahitaji hayo ni kwa matumizi ya majumbani, viwanda-ni, biashara na Taasisi. Kwa sasa Mamlaka hiyo inazalisha lita milioni 46.5 ambazo ni sawa na wastani wa asilimia 58. Anabainisha changamoto kubwa ambayo imepunguza kiwango cha uzalishaji wa maji kuwa ni shughuli za ki-jamii pamoja na mabadiliko ya tabia nchi yaliyopelekea kushuka kwa uwezo wake wa uzalishaji Maji katika maeneo ya vyanzo vya maji.

"Mamlaka ina jumla ya vyanzo 16 vyenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 59.95 kwa siku. Vyanzo hivi vimeathiriwa na shughuli za kijamii pamoja na mabadiliko ya tabia nchi na kupelekea kushuka kwa uwezo wake wa uza-lishaji na kufikia lita milioni 46.5. Hali hii imesababisha uzalishaji kuwa asili-mia 58 kwa siku ukilinganisha na mahitaji ya maji ya lita milioni 80 kwa siku". Kayange anasema.

Anaongeza pamoja na changamoto hizo bado wamejipanga wamejipanga kuhakikisha wanatatua changamoto zote zinazokwamisha kufikiwa kwa ma-lengo.
Anafafanua kuwa mkoa wa Mbeya unavyo vyanzo vingi vya maji ambapo wamebainisha vyanzo sita ambavyo wamejipanga kuhakikisha vinawavusha hadi kufikia malengo ya serikali ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani.

Anavitaja vyanzo hivyo kuwa ni chanzo cha maji cha Mwashali ambacho ki-natarajia kuhudumia eneo la Isyesye milimani pamoja maeneo ya Lyoto, Ilemi na Isyesye viwanja vipya.

Mradi huu ambao unatekelezwa kwa awamu mbili tofauti unatarajia kuwezesha Mamlaka kukusanya kiasi cha Shilingi Milioni 50 kwa Mwezi ma-ra baada ya kukamilika.

Eneo la pili linahusisha mradi wa maji wa Nzovwe – Isyesye uliosanifiwa ili kuondoa kero ya upatika-naji wa maji katika eneo la Isyesye ambalo kwa sasa huduma ya maji ni kwa mgao wa takribani saa



*Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akikagua chanzo cha maji cha mradi wa maji Nzovwe Jijini Mbeya.*

mbili hadi nne kwa siku.

Mradi huu unatarajiwa kuwahudumia wakazi wa Shewa, Ituha na Mwakibete kwa kuunganisha katika bomba linalopita eneo la SAE kuelekea Ituha.

"Mradi wa Nzovwe – Isyesye unatarajia kuhudumia wananchi wapatao 30,000. Aidha, Mradi huu unategemewa kuzalisha lita milioni 5 kwa siku. Vi-le vile Mradi huu unatarajia kuongeza makusanyo kwa Shilingi Milioni 250 kwa mwezi." Mkurugenzi Kayange anasema na kuongeza kuwa gharama za mradi ni Sh. Milioni 600 ambapo Serikali imetoa Sh. milioni 200 na Mam-laka imetumia mapato yake kiasi cha shilingi milioni 400.

Eneo lingine ni mradi wa maji Mbalizi ambao unapata maji kutoka chanzo cha Mto Shongo ambao umekamilika kwa asilimia 100. Mradi huu unazalis-ha lita milioni 10,000 kwa siku. Gharama za mradi ni Bilioni 3.345 ambapo Serikali Kuu iimetoa shilingi milioni 300 na Mamlaka kutumia mapato yake kiasi cha shilingi bilioni 3.045.

Mradi huu unahudumia wananchi wapatao 80,000 wa mji wa Mbalizi. Aidha, Mradi unachangia Mamlaka wastani wa mapato ya Sh. Milioni 75 kwa mwe-zi.

Mradi wa maji wa Ntangano ambao unatarajia kugharimu Sh. milioni 400 zitakazotokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka. Mradi huu unalenga kuhudumia wakazi wapatao 845 wa eneo la Ikanga, Mwahala na Iganjo. Mradi unatarajiwa kukamilika Julai, 2021.

Mradi wa Maji wa Mto Ilunga ambao unatarajia kugharimu Sh. 4.7 bilioni na utahudumia wakazi wapatao 140,000 wa eneo la Mji wa Mbalizi na eneo la Iwambi. Ukikamilika unatarajia kunufaisha watu 60,000.

Pia Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Chanzo cha Mto Kiwira ambao unakadiliwa kugharimu Sh. Bilioni 250. Mradi unatarajia kuongeza uwezo wa kuzalisha maji kwa kuongeza lita Milioni 87 na kuhudumia wakazi wa Jiji la Mbeya wapatao 750,000.

Kukamilika kwa Miradi hii kutaondoa kabisa changamoto ya uhaba wa maji katika Jiji la Mbeya na Mji Mdogo wa Mbalizi.

Mkurugenzi Kayange anaishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa miradi ambapo baadhi ya miradi inatekelezwa kwa ku-watumia wataalamu wa ndani wakati miradi mingine inatekelezwa kwa ku-watumia wakandarasi. Anasema wakandarasi wazembe hawana nafasi ka-tika utekelezajin wa jkiradi mkoani Mbeya.

Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Maryprisca Mahundi anapongeza jitihada kubwa inayofanywa na Mkoa huo hasa suala la ushirikiano katika utekeleza-ji wa miradi. Anasema siri kubwa aliyojifunza tangu aanze ukaguzi wa mi-radi katika mkoa huo ni ushirikiano kati ya Mamlka ya Maji, RUWASA na wadau wengine wa Maji. Anasema hii ndiyo Siri kubwa ambayo mikoa min-gine inatakiwa kujifunza.

# Mafanikio RUWASA, Takwimu zaongea

Mwaka 2019 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Wa-kala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Moja ya lengo ilikuwa ni kuhakikisha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi inaimarishwa zaidi hasa vijijini.

Uamuzi huu uliienda sambamba na kubadilisha mfumo wa uwajibikaji kwa kuwahamisha watumishi wa halmashauri kati-ka sekta ya Maji,kwenda Wiza-ra ya Maji .

Baada ya uamuzi huu Watanzania sehemu mbalimbali walian-za kuweka matumaini makubwa kwa RUWASA huku baadhi wakiwa na mashaka ya uchanga wao katika kufikia malengo ndani ya kipindi kifupi. Leo hii ni ta-kribani miaka miwili tan-gu RUWASA ianzishwa. Wananchi wanao ushuhuda mwingi wa kupima mafanikio ya RUWASA.

Wakati wananchi wakiendelea na tafakari yao kuhusu RUWA-SA, Septemba 6, 2021 Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) alikutana na viongozi wa RUWASA . Tukio hilo liliwaweze-sha RUWASA kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi tangu kuanzishwa lilirushwa Mubashara kupitia channel ya youtube ya majiDital kutokea ofisi za Wizara zilizoko mji wa Serilali, Mtumba jijini Dodoma.

Taarifa hiyo ilibainisha mambo mengi ambayo yanatoa matu-maini makubwa ya kuyafikia malengo yaliyoko katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo inatekelezwa na serika-li. Ilani hiyo inaitaka serikali hadi kufikia mwaka 2025 huduma ya Maji vijijini ifikie asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mi-jini.

Mwezi Julai, 2019 baada ya kuanzishwa kwa RUWASA wali-pokea miradi 632 iliyokuwa ikitekelezwa na halmashauri za wilaya. Miradi hiyo ilikuwa katika hatua mbalimba;li za ute-kelezaji. Hadi kufikia Juni 2021 Jumla ya miradi 566 sawa na asilimia 89.6 tayari ilikuwa imeshakamilishwa na kutoa hudu-ma sehemu mbalimbali katika vijiji vya Tanzania.

Aidha, ipo miradi ambayo ilikuwa imekamilika lakini ilikuwa haitoi huduma ya majisafi. Miradi hii ndiyo ambayo mara kad-haa Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso amesikika akii-ta miradi sugu na kutangaza kuhakikisha ina-kwamuliwa kwa haraka.

Taarifa kuhusiana na sababu za kukwama kwa miradi hii in-abainishwa kuwa ipo miradi ambayo ilibuniwa bila kufanyiwa utafiti wa kina hali ambayo ilisababisha maji yasitoke, au yatoke kwa muda mfupi kisha kukata. Pia ipo miradi ambayo mashine zake zilikumbwa na changamoto ya kuharibika ma-ra kwa mara kutokana na sababu za kijiografia. Miradi mingine ilikwama kwa sababu ya kutopata umeme unaotosheleza.

Aidha, Miradi mingine ilikuwa haitoi huduma kutokana na changamoto ya usimamizi wenye shaka au wananchi wa mae-neo husika kuiba vifaa au kutokutoa ushirikinao katika usima-mizi wa miradi hiyo.

"Kama ni suala la wizi, ubadhirifu wa mali toka kwa wanan-chi, umeme na mengine yote hatuwezi kushindwa wakati sisi ni serikali. Tunavyo vyombo vya ulinzi na usalama, Wananchi wema wanaoitakia mema serikali wapo. Yote haya yako ndani ya uwezo wetu. Lazima tupambane kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya majisafi na salama katika eneo lake, Wizara ya Maji haiwezi kuwa kikwazo kwa wananchi kupatqa huduma" Waziri Awe-so amenukuliwa mara kwa mara akisema haya.

Idadi ya miradi hiyo iliyobainika ni miradi 177. Hadi Juni 21,



*Mkurugenzi Mkuu RUWASA Mhandisi Clement Kivegalo pamoja na Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) wakishiriki ujenzi wa mradi wa maji wilayani Chunya mkoani Mbeya*

2021 jumla ya miradi 115 sawa na asilimia 65 ilikuwa imekamilishwa na kutoa huduma kwa wananchi. Miradi 62 iliyobaki imewe-kwa katika utaratibu wa kukamilika kati-ka mwaka wa fedha 2021/2022.

Pia ipo miradi ambayo ilianza kutekelezwa na RUWASA mara baada ya kuanzishwa. Jumla ya miradi hiyo ni 912 ambapo hadi Juni 21, 2021 RU-WASA imeweza kukamilisha mi-radi 458. Pia RUWASA ilipanga kuanzisha skimu za maji 912 ambapo skimu 666 zime-kamilika na kuwezesha jumla ya vijiji 1673 vyenye wananchi wapatao 3,820,180 kupata vituo vya kuchotea maji 11,421 ambapo vi-meweza kuongeza upatikanaji wa Maji kwa asilimia 1.93.

Kwa upande wa usimamizi wa maji kati-ka ngazi ya jamii, RUWASA inatam-bua umuhimi wa kuwa na wataalamu na usimam-izi imara katika ngazi ya watumia maji hivyo mara baada ya kuanzishwa iliamua kuhuisha, kuanzisha na kusajlii jumuia za watumia maji (CBWSOs) 2410 kati ya 3256 ili usimam-zi wa maji uwe mzuri na endelevu. Kuanzish-wa kwa jumuia hizo kumeonge-za ajira kwa jamii ambapo wataalamu 1694 wameajiriwa na Jumuia hizo. Walioajiriwa ni mafundi 906 na 788 ni wahasibu.

Jumuia hizi zimepewa vitendea kazi ikiwe-mo usafiri kwa lengo la kurahisisha shughuli. Hadi Juni 2021 Jumuia za watumia Maji 44 zinatumia usafiri wa magari, Jumuia 146 zi-natumia usafiri wa Pikipiki wakati Jumuia 22 zinatumia usafiri wa baiskeli.

Lengo ni kuhakikisha kila jumuia inakuwa katika mzingira mazuri ya usimamzi kupitia us-afiri na wataalamu katika eneo husika.

Takwimu za mafanikio ya RUWASA ni nyingi na zinawapa nafasi ya kuongeza jitihada zaidi kwani muelekeo unaonesha mafanikio katika kuondoa changamoto ya upatikanajni wa majis-afi na salama kwa wananchi.

Kwa yale maeneo ambayo wanapata huduma ya Maji kwenye vituo vya ku-chotea maji msisitizo umewekwa kuwataka wananchi wasogeze maji kwenye majumba yao kama ilivyo kaulimbiu ya RUWASA ya 'Maji bombani'. Maji yawafikie wa-nanchi katika nyumba zao.

Mipango ya RUWASA ni kuhakikisha miradi ya kimkakati 100 inatekelezwa ili kuleta matokeo chanya kwa jamii.

Utekelezaji wa miradi kwa kuwatumia wata-alamu wa Wizara umepewa msisitizo kwani imewezeshwa kwa kiasi kikubwa kuharakisha utekelezaji wa miradi na kupunguza gharama za utekelezaji. Pia imebainika kuwa utaratibu huo umewezesha miradi kutekelezwa kwa kutumia vifaa vyenye ubora sta-hili na kuwawezesha watalamu wa Wizara kuwa na uzoefu wa kute-keleza miradi mikubwa.

Kwa kuzingatia hilo, takwimu zinaonyesha kuwa RUWASA imepanga kutele-leza jumla ya miradi 1179 katika mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo mira-di 397 itatekelezwa na wataalamu wa RU-WASA kwa utaratibu wa 'Force Ac-count' aidha miradi 779 itatekelezwa na wakandarasi

# Iringa washukuru kwa Dira za Malipo Kabla



*Dira za malipo kabla zikiwa zimefungwa katika moja ya eneo la biashara mjini Iringa*

Huduma ya majisafi kwa kutumia Dira za Malipo Kabla (LIMAKU) imeleta mwamko mkubwa kwa wakazi wa mjini Iringa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) Mhandisi David Pallangyo amesema kwa kuanzia asilimia 15 ya wateja wa IRUWASA wamefungiwa LIMAKU.
Mhandisi Pallangyo amesema matumizi ya Dira hizo yamesaidia wateja mambo kadhaa ikiwamo; kulipa kadri wanavyotumia, na kuepuka foleni za kuangalia madeni au kufanya malipo. Aidha, wateja wamewezeshwa kufanya malipo au kuhamisha kiasi cha maji waliyonunua, hivyo kurahisisha matumizi.

Amesema Dira hizo zimefungwa katika maeneo yanayotoa huduma kwa umma ikiwamo baadhi ya shule na vyuo, migahawa na baadhi ya wateja na kazi hiyo ni endelevu kwa sababu matumizi ya Dira hizo yanapunguza gharama za uendeshaji.

Mkurugenzi Pallangyo anasema huduma ya LIMAKU ilipoanza ilibidi kutoa elimu kwa wateja kuhusu matumizi sahihi.

Amesema, kufuatia mwitikio mkubwa kwa wateja, IRUWASA imejipanga kuhakikisha huduma inawafikia wananchi na wameagiza Dira za LIMAKU 5000.

“Maombi ya kufungiwa LIMAKU yanaongezeka kila siku.
Sisi kama mamlaka tumeagiza Dira 5000 ili kuhakikisha tunakidhi huduma hiyo hatua kwa hatua,” Mhandisi Pallangyo amesema.

Kwa upande wake, Mstahiki Meya wa Halmashauri Manispaa ya Iringa, Mhe. Ibrahimu Ngwada amesema huduma ya majisafi inagusa sehemu kubwa ya maisha ya wakazi wa Iringa, hivyo amevutiwa na IRUWASA kuhusu mbinu za kurahisisha huduma ya upatikanaji wa majisafi kwa wananchi

“Tunashirikiana vizuri na IRUWASA katika kazi hii ya huduma ya maji. Tunaishukuru serikali kwa kuja na matumizi ya teknolojia hii ya malipo kabla, huduma inawafundisha wakazi wa Iringa kutumia maji kwa uhuru majumbani mwao kadri wanavyohitaji, Mhe. Meya Ibrahimu Ngwada anasema.

Naye Mkufunzi na Msimamizi wa miundombinu ya maji katika Chuo cha Ufundi Stadi Mkoa wa Iringa VETA, Bw. Karolo Magani anafafanua huduma hiyo imeweza kuwasaidia katika kupunguza upotevu wa muda katika kulipia bili za maji, na kubaini kwa haraka endapo kuna hitilafu ya miundombinu ya mfumo wa maji chuoni hapo.

“Tangu chuo chetu tufungiwe Dira hizi za malipo kabla, kumekuwa na mabadiliko makubwa sana katika matumizi ya majisafi, imesaidia kufahamu kama kuna uvujaji wa maji katika miundombinu yetu. Pia, tumeondokana na foleni za kulipa kila mwisho wa mwizi”
, Magani anasema.

Mmoja ya wakazi wa mjini Iringa Tadeus John ambaye anatumia LIMAKU anatoa ushuhuda kuwa matumizi ya Dira hizo yamesaidia kufahamu kiasi cha majisafi ambacho familia yake inatumia na pia kujiepusha na kulimbikiza bili za huduma ya maji.

“Tangu nianze kutumia huduma ya hii ya malipo kabla nimeona mabadiliko haswa katika swala la matumizi ya maji,nimetambua familia yangu inatumia kiasi gani cha majisafi na utamaduni uliokuwepo awali wa kulimbikiza madeni ya biliza majisafi kwa sasa haupo”. alisema Tadeus John







Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), akiwa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), pamoja na watendaji wengine wa wizara ya maji, wakati wa ukaguzi wa Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe . Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa katika ukaguzi wa mradi alielekeza iangaliwe namna bora ya kumalizia kazi zilizobaki kwa wakati katika mradi huo



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akimkabidhi nyaraka za utendaji kazi Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) Mhandisi Cyprian Luhemeja, mara baada ya kuzindua Bodi ya wakurugenzi wa DAWASA. Mhandisi Luhemeja ni Katibu wa Bodi hiyo, na hafla ya uzinduzi ilifanyika makao makuu wa DAWASA, jijini Dar es salaam.




Mama Mhandisi, Mshindi: Mkurugenzi Msaidizi, Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri (katikati) akiwa na Tuzo ya Mwaka ya Mama Mhandisi 2021




# Usikose kufuatilia vipindi vya Maji ni Uhai katika kituo cha Runinga cha Channel Ten.



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba akikagua kazi ya kusambaza mabomba katika mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe. Kazi hiyo inafanywa na mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) na katika mji wa Mwanga mabomba yamelazwa kilometa 49 kati ya kilometa 53 na Same kilometa 3 kati ya 15. Kazi inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2021



*Mmoja kati ya wataalamu wa ndani wanaounda Kikosi kazi, akikagua mfumo wa umeme katika mradi wa maji wa Makonde. Mradi huo unafanyiwa ukarabati mkubwa baada ya kukaguliwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga ambaye ameunda kikosi kazi kwa ajili ya kazi ya ukarabati mkubwa*



*Mafundi wakiendelea na kazi ya kuunga mabomba yanayolazwa ili kufikisha huduma ya majisafi kwa wananchi katika mradi wa maji wa Same-Mwanga –Korogwe*



*Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira CPA Joyce Msiru (kulia) akiwa pamoja na timu iliyotekeleza ujenzi wa mradi wa maji wa Darakuta - Magugu, wakitembea kuelekea katika dakio la maji la mradio huo*



Kitengo cha Mawasiliano

Tovuti: www.maji.go.tz